



TAARIFA KWA UMMA

KUKAMILIKA KWA AWAMU YA TATU YA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Dar es Salaam, Tarehe 2 Oktoba, 2021

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa Awamu ya Tatu ya Udahili kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2021/2022 umekamilika. Majina ya waombaji waliodahiliwa katika Awamu ya Tatu yanatangazwa na vyuo husika.

2.0 WAOMBAJI WALIODAHILIWA KATIKA CHUO ZAIDI YA KIMOJA


Waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale ambao hawakuweza kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita wanasisitizwa ***kuthibitisha udahili wao katika chuo kimojawapo kuanzia tarehe 3 hadi 24 Oktoba, 2021*** kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba zao za simu au barua pepe walizotumia wakati wa kuomba udahili. Wale ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia kwenye mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa na kuomba kutumiwa ujumbe mfupi wenye namba maalum ya siri ili kuweza kujithibitisha katika chuo husika. Aidha, uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo muombaji alitumia wakati wa kuomba udahili.

Orodha ya majina ya waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika Awamu ya Tatu na wale ambao walishindwa kuthibitisha udahili katika awamu zilizopita imewekwa katika tovuti ya TCU (www.tcu.go.tz).

3.0 WITO KWA WAOMBAJI UDAHILI

Waombaji udahili wa Shahada ya Kwanza wanakumbushwa kuwa masuala yote yanayohusu udahili au kujithibitisha katika chuo kimoja yawasilishwe moja kwa moja kwenye vyuo husika.

Imetolewa na:


Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA